# TFRA na MATUKIO

Toleo Na. 1 | Tanzania Fertilizer Regulatory Authority | tfra_official | tfra_official | Aprili 2022

JARIDA LA MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA


## SERIKALI KUONDOA UZEMBE NA VITENDO VYA RUSHWA MAHALA PA KAZI



Mwenyekiti wa bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Prof. Anthony Mshandete akizungumza na Menejimenti na wajumbe wa Baraza la wafanyakazi wa Mamlaka hiyo alipokuwa akifungua kikao cha pili cha baraza la wafanyakazi wa mamlaka kilichofanyika tarehe 25 Februari,2022 katika ukumbi wa Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) mkoani Morogoro.

NDANI>>


TFRA YAFIKIA ASILIMIA 93 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YAKE 6

TFRA YATOA ELIMU MATUMIZI SAHIHI YA MBOLEA MIKOA YA KUSINI 8

WAZIRI BASHE ATAKA TAASISI ZA KILIMO ZISHIRIKIANE 10

# Kuanzishwa Jarida la "TFRA na MATUKIO"

Ni furaha ilioje kama taasisi kuwatangazia washirika na wadau wetu kwamba sasa tumeanzisha jarida la mtandaoni litakaloitwa "TFRA News Bulletin" litakalokuwa likisheheni habari motomoto za matukio mbalimbali yanayotokea kila mwezi katika tasnia ya mbolea nchini.

Tumechukua uamuzi huu tukielewa wazi kwamba tasnia ya mbolea ni muhimu kwa uchumi wa taifa na kasi ya ukuaji inaongezeka siku kwa siku hivyo wananchi, hasa wakulima, wana kila sababu ya kufahamu matukio muhimu yanayotokea katika sekta hii kupitia utekelezaji wa majukumu ya udhibiti wa mbolea nchini.

Leo hii serikali inavyotilia mkazo uimarishaji wa sekta ya kilimo, yapo mambo mengi yanayotokea katika tasnia ya mbolea ambayo washirika, wadau na wakulima wanapaswa kuyafahamu. Hii ni kwa sababu katika miaka ya hivi karibuni mbolea imeleta matokeo chanya katika kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali nchini.

Katika jarida hili la TFRA News Bulletin tutakuwa tukiwaletea habari za mbolea kutoka mikoa iliyosheheni shuhuda za wakulima waliotajirika kutokana na matumizi sahihi ya mbolea na changamoto nyingine za upatikanaji wa bidhaa hiyo nchini.

Katika jarida hili tutapenda kupokea maoni mbalimbali ya wadau wetu ambayo yatasaidia Mamlaka na taifa kwa ujumla kujua mafanikio na changamoto zilizopo katika kukuza tasnia ya mbolea. Lazima tuelewe kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo wa taifa letu na kwamba mbolea ni kichocheo kikubwa kitakachokuza sekta hiyo na kuimarisha uchumi wa taifa.

Tunawakaribisha kutoa maoni kutoka kwa wadau mbalimbali ili yatusaidie kuboresha udhibiti na matumizi sahihi ya mbolea.

**Tumia mbolea kwa kuongeza tija katika uzalishaji**

**Karibuni!**




***Anuani:***
***Wizara ya Kilimo***
***Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA)***
***Mtaa wa Kilimo, Jengo la Kilimo,***
***S.L.P 46238 DAR ES SALAAM***
***+255 22 2861939***

Tanzania Fertilizer Regulatory Authority    tfra_official    tfra_official

# Serikali kuondoa uzembe na vitendo vya rushwa mahala pa kazi

Imeelezwa kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mh. Rais Samia Suluhu Hassan imedhamiria kwa dhati kuondoa uzembe na vitendo vyovyote vya rushwa mahala pa kazi ikiwa ni pamoja na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili kuongeza tija kwa taifa.

Hayo yamebainishwa leo, tarehe 25 Februari, 2022 na Prof. Anthony Mshandete Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea wakati akifungua kikao cha pili cha Baraza la Wafanyakazi cha Mamlaka hiyo kilichofanyika katika ukumbi wa Mviwata Mkoani Morogoro.

Kufuatia nia hiyo ya dhati ya Serikali, Prof. Mshandete amesema ni wajibu wa kila mfanyakazi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kuhakikisha anafahamu wajibu wake mahala pa kazi na anatekeleza malengo aliyopangiwa katika muda uliopangwa, vile vile anatunza mali na vifaa alivyokabidhiwa kufanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuwahi kazini.

Amesema, Serikali inazingatia sana suala la taasisi zake kuwa na mabaraza ya Wafanyakazi kwani yanaanzishwa kisheria kwa



Mkurugenzi Mtendaji na Mwenyekiti wa Baraza la wafanyakazi wa TFRA akizungumza na wajumbe wa mkutano huo wakati wa kikao cha pili cha baraza la wafanyakazi wa mamlaka hiyo tarehe 25 Februari, 2022 mkoani Morogoro.

madhumuni ya kuishauri Serikali katika ngazi za idara, taasisi na wizara kuhusu usimamizi wa kazi na rasilimali watu, utekelezaji wa majukumu, kulinda haki na wajibu wa waajiri na Wafanyakazi, kutoa ushauri kuhusu kujenga hali bora mahali pa kazi, maslahi ya wafanyakazi na kusimamia haki na ustawi mahali pa kazi.

Ameongeza kuwa, wajibu wa mabaraza haya kama vyombo vya ushauri na usimamizi ni kuhakikisha kuwa waajiri na watumishi wanatambua wajibu na haki zao, pia wanazingatia maadili ya utumishi wao kwa umma ili kuleta matokeo ya utendaji wa kazi yenye tija, staha na upendo.

Prof. Mshandete amesema, kufuatia lengo la kikao hicho la kuwawezesha wafanyakazi kupitia utekelezaji wa nusu mwaka wa bajeti ya TFRA ya mwaka wa fedha wa 2021/2022 na kupitia makadirio ya Bajeti ya Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2022/2023 mamlaka hiyo itakuza uwazi na ushirikishwaji katika maamuzi mbalimbali ya Mamlaka na kuwafanya watumishi kutekeleza majukumu yao wakiwa na uelewa mpana wa Mpango Mkakati wa Mamlaka kwa Miaka mitano yaani 2021/2022 hadi 2025/2026.

Pamoja na hayo, Prof. Mshandete amesema kikao

# Serikali kuondoa uzembe na vitendo vya rushwa mahala pa kazi

hicho kitamfanya Mfanyakazi wa TFRA kufahamu kuwa anatakiwa kutoa huduma ya kiwango gani kwa mteja mara kwa mara. Wakati huo huo ni lazima ajue bajeti iliyotengwa kwa ajili ya shughuli zake ndani ya Mamlaka ili afanye kazi kwa kuzingatia malengo na rasilimali zilizokadiriwa kutumika.

Nichukue fursa hii kuwataka wafanyakazi wa TFRA kufuata utaratibu unaoelekezwa na bajeti yenu. Tutakapokuwa tunafanya mapitio ya bajeti ya nusu mwaka hapo baadae, tutaona ni nani au Idara gani haikufanya kazi kulingana na malengo ya Mamlaka.

“Sisi kama Bodi, hatutasita kumwajibisha Mkurugenzi wa Idara au Meneja yeyote kati yenu ambaye ataonekana kuwa chanzo cha kutotimiza malengo ya Bajeti na Mpango kazi wa Mamlaka” Prof. Mshandete amekazia.

Aidha, Prof. Mshandete amewataka uongozi wa Menejimenti ya Mamlaka na Chama cha wafanyakazi kuwa na mshikamano thabiti wakati wote ili kuweza kutimiza majukumu yao ipasavyo na kuifanya bodi kutimiza majukumu ya kuisimamia mamlaka hiyo ipasavyo. “Kama mtakuwa na migongano kati ya Menejimenti na TUGHE ufanisi wa kazi hautaonekana na hivyo kuifanya Bodi ishindwe kutimiza azma yake ya kuisimamia vizuri Mamlaka” Prof. Mshandete alikazia.



Katibu wa Baraza la Wafanyakazi Tawi la TFRA akizungumza na washiriki wa Mkutano wa Baraza uliokaa hivi karibuni mkoani Morogoro.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa TFRA na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi Dkt. Stephan Ngailo amesema Baraza la wafanyakazi ni takwa la kisheria lililoundwa kwa Sheria ya Majadiliano ya Utumishi wa Umma Na.19 ya Mwaka 2003 na Sheria ya ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya Mwaka 2004 pamoja na Sheria ya Asasi za kazi Na. 7 ya Mwaka 2004.

Ameongeza kuwa kikao cha Baraza la Wafanyakazi kwa TFRA kinachofanyika mkoani Morogoro ni cha pili kufanyika tangu mamlaka ianze kazi ya udhibiti wa mbolea mnamo mwaka 2012 baada ya kili kilichofanyika tarehe 4 na 5 ya Mwezi wa pili Mwaka 2021 Jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika kikao hicho Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi tawi la TFRA Azizi Mtambo aliwataka wajumbe wa kikao hicho kushiriki kikamilifu katika kikao hicho kwa kutoa hoja zitakazoongeza tija katika utendaji wa mamlaka na si kuhudhuria tu kikao hicho.

# HABARI PICHANI



















Matukio mbalimbali katika picha wakati wa kikao cha baraza la wafanyakazi kilichofanyika tarehe 25 Februari, 2022 Mkoani Morogoro.

# TFRA YAFIKIA ASILIMIA 93 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YAKE

Imeelezwa kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imefikia asilimia 93 ya utekelezaji wa majukumu ya mamlaka hiyo kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Julai mpaka Desemba 2021 kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Hayo ni mafanikio makubwa kwa taasisi ambapo bado imeweka mikakati na malengo ya kuhakikisha inatekeleza majukumu yake kwa asilimia mia moja.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania Dkt. Stephan Ngailo akizungumza jambo wakati wa kikao cha wafanyakazi na watendaji wa mamlaka hiyo kilichofanyika tarehe 11 Februari, 2022 katika viwanja vya mamlaka hiyo eneo la Kilimo Jijini Dar es Salaam.

Hayo yamebainishwa tarehe 11 Februari, 2022 na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Dkt. Stephan Ngailo alipokuwa akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi kwa kipindi cha tajwa kwa watumishi wa TFRA katika kikao cha kawaida cha wafanyakazi kinachofanyika kila robo ya muhula ya mwaka wa fedha.



Mkurugenzi wa Huduma za Mamlaka Bi. Victoria Elangwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa mamlak hiyo kwa kipindi cha nusu mwaka wakati wa kikao cha wafanyakazi na watendaji wa mamlaka hiyo kilichofanyika tarehe 11 Februari, 2022 katika viwanja vya mamlaka hiyo eneo la Kilimo Jijini Dar es Salaam.

Pamoja na kueleza mafanikio hayo, Dkt. Ngailo amewapongeza watumishi wa Mamlaka hiyo kwa mchango wao katika kufikia mafanikio hayo na kuwataka kuimarisha mawasiliano na mahusiano miongoni mwao ili kuboresha utendaji na kuifanya Mamlaka ifikie malengo iliyojiwekea.

“Kila mmoja ana mchango wa kumfanya mwingine atekeleze majukumu yake

# TFRA YAFIKIA ASILIMIA 93 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YAKE

hivyo tufanye kazi kwa kutegemeana na tupafanye mahala pa kazi kuwa ni mahala salama na mahala pa kupafurahia" Dkt. Ngailo alisisitiza.

Akikazia kuhusu suala la udhibiti ubora wa mbolea ikiwa ni jukumu mama la Mamlaka hiyo, Dkt. Ngailo amewataka maafisa udhibiti kuhakikisha wanaimarisha shughuli za udhibiti wa mbolea katika maeneo yao ya kazi na kuhakikisha mbolea inayoingia na kutoka nchini inakidhi viwango vya ubora vinavyokubalika na hivyo kuleta matokeo chanya kwa wakulima nchini.

Aidha, Dkt. Ngailo amewataka watumishi wa Mamlaka hiyo kutokujihusisha na masuala ya ulevi wakati wa kazi na kusisitiza suala la ulevi kazini halikubaliki. "Niwaombe sana mameneja wa kanda mzingatie suala la maadili kazini hasa ulevi wakati wa kazi, nizamu ni lazima" Dkt. Ngailo alisisitiza.

Mwisho Dkt. Ngailo amewataka mameneja wa kanda kuwa na mahusiano mazuri na viongozi wa mikoa na wilaya katika kanda wanazozisimamia. "Mwende mkashirikiane kikamilifu na wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, watendaji wote katika ngazi za mikoa na wilaya pamoja na wadau wote wa sekta ikiwemo wakulima, wazalishaji na wafanyabiashara wa mbolea" Dkt. Ngailo alikazia.

Kwa Upande wake Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi, Victoria Elangwa amesema Mamlaka ipo katika hatua nzuri ya utekelezaji wa majukumu lakini inaendelea kuboresha mpango mkakati wake ili uendane na mpango mkakati wa Taifa na hivyo kugusa kikamilifu agenda za kitaifa katika kuwaletea maendeleo watanzania.

Akitoa taarifa ya kikao cha bodi ya wakurugenzi ya Mamlaka hiyo kwa watumishi wake, Elangwa amesema Bodi imeridhishwa na utendaji wa Mamlaka kutokana na kusimamia na kutekeleza majukumu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali inayosimamia Mamlaka hiyo.

Pamoja na hayo, Elangwa amewasihi watumishi hao, kubuni mbinu za kuongeza vyanzo vya mapato vya taasisi huku kila mmoja akiendelea kuboresha utendaji katika eneo lake la kazi.

Kikao hiki ni cha pili kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambapo Mamlaka imejiwekea utaratibu wa kufanya vikao kila robo ya Mwaka ili kujifanyia tathmini ya utendaji wa kila siku wa Mamlaka na kurekebisha kasoro zinazojitokeza na kukwamisha utendaji.



Watumishi wa TFRA wakifuatilia mada wakati wa kikao baina yao na watendaji wa mamlaka hiyo ikiwa ni utaratibu wa mamlaka hiyo kuwa na vikao na watumishi kila kipindi cha robo ya utekelezaji wa majukumu ya mamlaka.

# TFRA YATOA ELIMU MATUMIZI SAHIHI YA MBOLEA MIKOA YA KUSINI

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara imetoa elimu kwa vitendo kupitia mashamba darasa kwa ajili ya kuhamasisha matumizi sahihi ya mbolea kwa lengo la kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya mahindi na mpunga.

Katika jitihada zake za kuhamasisha matumizi sahihi ya mbolea kwenye mikoa hiyo serikali kupitia TFRA imeanzisha mashamba darasa katika halmashauri za Ruangwa, Mtama, Mtwara na Masasi ambapo wakulima kupitia vikundi vyao wamepata elimu ya matumizi sahihi ya mbolea kwa njia ya vitendo.

Akitoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea katika halmashauri hizo, Afisa Udhibiti Ubora kutoka TFRA Aziz Mtambo amesema mkulima hawezi kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao shambani pasipo kutumia mbolea.

Mtambo amesema ili mmea ukue na kutoa mavuno bora shambani unahitaji virutubisho vya kutosha na virutubisho hivyo hupatikana



Kikundi cha wakulima wa kijiji cha Chimbila B katika halmashauri ya wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi wakifanya palizi katika Shamba darasa kwa ajili ya uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea

kwenye udongo wenye rutuba ya kutosha.

Ameongeza kuwa upungufu wa virutubisho unapotokea shambani huhitajika kuongezwa kwa kuweka mbolea ambayo amesema huwa na virutubisho mbalimbali ikiwemo naitrojeni, fosiforasi na potasiamu.

Mtaalamu huyo amesema kuwa mambo muhimu anayotakiwa kuzingatia mkulima kabla ya kuweka mbolea ni pamoja na afya ya udongo wa shamba, aina ya mbolea itakayotumika na upatikanaji wa mbolea husika.

Amesema matumizi sahihi ya mbolea ni lazima yazingatie kanuni bora zingine za kilimo ikiwemo kuandaa shamba kwa wakati, matumizi ya mbegu bora, kupalilia, kupiga madawa ya kuzuia na kuua wadudu na magonjwa mbalimbali na kuvuna kwa wakati unaostahili.

“Ni vema wakulima mkafahamu kuwa matumizi sahihi ya mbolea ni pamoja na kutumia mbolea sahihi, kiwango sahihi , wakati sahihi na sehemu sahihi ili kuleta matokeo mazuri yatakayoongeza tija katika uzalishaji wa mazao”, alisema Mtambo.

Naye Afisa Kilimo wa Kata ya Kitere iliyopo katika halmashauri ya wilaya ya Mtwara Swalehe Tendwa amesema kupima afya ya udongo inasaidia kutambua virutubisho vilivyopo kwenye udongo na vipo kwa kiasi

# TFRA YATOA ELIMU MATUMIZI SAHIHI YA MBOLEA MIKOA YA KUSINI

gani na uchachu uliopo.

Tendwa ameongeza kuwa faida za kupima afya ya udongo ni pamoja na kupunguza gharama za uzalishaji kwani mkulima atanunua mbolea kulinganana upungufu uliopo kwenye udongo wa shamba lake na kutambua kiwango sahihi cha mbolea kinachohitajika.

Aidha amesema uhamasishaji wa matumizi ya mbolea unaofanywa na TFRA kwa kushirikiana na mikoa ya Lindi na Mtwara umeleta mwamko mkubwa kwa wakulima katika msimu huu wa kilimo ambapo wananchi wengi wamekuwa wakipita katika mashamba darasa hayo ili kujifunza faida za kutumia mbolea katika uzalishaji wa mpunga na mahindi.

Kwa upande wake Mkuu wa wilaya ya Lindi Shaibu Ndemanga akizungumza wakati wa uzinduzi wa mashamba darasa hayo hivi karibuni alisema kuanzishwa kwa mashamba hayo kutaleta hamasa kubwa kwa wakulima wa mikoa hiyo kutaka kutumia mbolea katika uzalishaji wa mazao mbalimbali na hivyo kuongeza kipato.

Amesema mikoa ya Lindi na Mtwara ina zaidi ya hekta 6,400, 000 zinazofaa kwa kilimo cha mazao mbalimbali, hata hivyo tija ya uzalishaji kwenye mazao mengi bado ni ndogo.

“Takwimu hizi zinaonyesha uwepo wa utajiri wa maeneo ya kutosha yanayofaa kwa kilimo cha mazao mbalimbali lakini bado hatujaweza kutumia fursa hii kwa ukamilifu na moja ya sababu ni kwamba wakulima wengi hawazingatii kanuni bora za kilimo ikiwemo matumizi ya mbolea,” alisema Ndemanga.

Mkuu wa wilaya huyo amesema mikoa ya Lindi na Mtwara kwa miaka iliyopita imekuwa ikikabiliwa na upungufu wa chakula, hivyo kusababisha serikali kuleta chakula cha msaada ili kupunguza kutokea kwa baa la njaa.

Mwenyekiti wankikundi cha wakulima cha Tupendane katika halmashauri ya wilaya ya Mtwara Bi. Mary Mapunda ameishukuru serikali kupitia TFRA kwa kuwaelimisha kwa vitendo kuhusu matumizi sahihi ya mbolea kwa kutumia mashamba darasa.

Bi. Mapunda amesema vikundi vya wakulima vimehamasika kushiriki katika hatua zote za mafunzo hayo kwa vitendo kwani elimu hiyo inawasaidia kuelewa kwa haraka kuhusu matumizi sahihi ya mbolea katika uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Wakulima zaidi ya 60 katika halmashauri za Ruangwa, Mtama, Masasi na Mtwara wanashiriki katika hatua zote zinazofanyika kwenye mashamba darasa hayo yenye lengo la kuhamasisha matumizi sahihi ya mbolea katika uzalishaji wa mazao ya mahindi na mpunga.



Wakulima wa Kata ya Kitele katika Halmashauri ya wilaya ya Mtwara wakipalilia Shamba darasa kwa ajili ya uhamasishaji wa matumizi sahihi ya Mbolea.

# Waziri Bashe ataka taasisi za kilimo zishirikiane kusababisha matokeo chanya kwenye Sekta

Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe amezitaka Wakala, Bodi za Mazao na Taasisi zilizo chini ya wizara kutumia fursa zilizopo kuleta mabadiliko chanya kwenye Sekta ya Kilimo.

Akizungumza baada ya kikao chake na Wakuu wa Wakala, Bodi za Mazao, Taasisi na Menejimenti ya Wizara kilichofanyika hivi karibuni Jijini Dodoma, Waziri Bashe alisema ili kuwa na matokea bora ni lazima wafanye kazi kwa ushirikiano ili kufikia malengo waliyojiwekea.



Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe, akizungumza na Wakuu wa Wakala, Bodi za Mazao, Taasisi na Menejimenti ya Wizara hiyo wakati wa kikao chake na viongozi hao kilichofanyika tarehe 22 Januari, 2021 Jijini Dodoma.

Miongoni mwa malengo aliyoyataja Waziri Bashe ni pamoja na kuongeza wastani wa ukuaji wa Sekta ya Kilimo kutoka asilimia 5 sasa hadi kufikia asilimia 10.



Baadhi ya Wakuu wa Wakala, Bodi za Mazao, Taasisi na Menejimenti ya Wizara wakifuatilia maelekezo kutoka kwa waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe wakati wa kikao kilichofanyika hivi karibuni Jijini Dodoma.

Akizungumzia moja ya malengo waliyojiwekea ili kuongeza tija kwenye Sekta ya Kilimo Mhe. Bashe alisema ni kuongeza wastani wa uuzaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi kutoka dola za marekani bilioni 1.2 hadi kufikia dola bilioni 5 kwa mwaka ujao.

Kuhusu kilimo cha umwagiliaji Mhe. Bashe aliwaagiza Watendaji hao kuhakisha kuwa mchango wa umwagiliaji katika uzalishaji unaongezeka hadi kufikia asilimia 50 kutoka aslimia 10 iliyopo sasa.

Mbali na kiwango cha uzalishaji wa mazao ya kilimo; Mhe. Bashe alisema haridhishwi na hekta laki sita zinazotumika katika kilimo cha umwagiliaji ikiwa nchi ina hekta milioni 29 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Pamoja na hayo, Waziri Bashe alibainisha kuwa malengo hayo yatafikiwa kwa kuchagua mazao machache ya kimkakati kutoka kwenye zaidi mazao 89 ambayo yanazalishwa Tanzania kwa sasa.

# TFRA yapongezwa usimamizi ujenzi maabara ya mbolea

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania kwa kuendelea kutekeleza jukumu lake la udhibiti wa mbolea huku ikitekeleza jukumu la ujenzi wa maabara ya mbolea ya kimataifa.

Mavunde ametoa pongezi hizo tarehe 26 Februari, 2022 alipotembelea Ofisi za mamlaka hiyo ili kukagua maendeleo ya ujenzi wa maabara hiyo inayotarajia kukamilika mwezi Mei, 2022 mradi uliopo katika eneo la Vetenari, kilimo three wilayani Temeke Jijini Dar es Salaam.

Naibu Waziri Mavunde alisema kuwa, kukamilika kwa maabara hiyo kutatoa fursa kwa tafiti za mbolea kufanyika nchini na matokeo yake kupatikana kwa wakati na hivyo kuwa mkombozi kwa wadau na wakulima kwa kupata mbolea kwa matumizi ya kilimo wakati wa msimu.

"Maabara hii itakuwa ni mkombonzi kwa masuala yote yanayohusiana na uchambuzi wa mbolea na wakulima watapata nafasi kuhudumiwa kwa wakati kutokana na matokeo ya upimaji wa mbolea kupatikana kwa wakati" Mvunde alisema.

Mavunde alisema pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na Mamlaka ni vema mamlaka hiyo ikahakikisha inafanya manunuzi ya vifaa vyote vinavyohitajika kwa ajili ya ujenzi mapema ili mkandarasi asikwame wakati wa utekelezaji wa mradi kutokana na kukosa vifaa hivo.

"Zipo njia za kurahisisha masuala ya manunuzi bila kukiuka matakwa ya kisheria, wasilisha mahitaji na ratiba yako kwa ajili ya ujenzi ili mamlaka iandae mahitaji hayo mapema" Mavunde alikazia.

Alisema, ujenzi wa maabara hiyo ni utekelezaji wa maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika kuboresha mazingira ya kusimamia na kudhibiti ubora wa mbolea nchini.

Akizungumzia manufaa ya maabara hiyo, Mavunde alisema maabara inayojengwa itawasaidia wadau wa mbolea katika kupata majibu ya uchambuzi kwa wakati aidha itapunguza gharama ya mbolea kutokana na bei ya bidhaa hiyo kuongezeka kutokana na kucheleweshwa kwa majibu ya uchambuzi yaliyokuwa yakifanywa na vyombo binafsi na hivyo kuongeza gharama ya kutunza mzigo bandarini.

Akizungumza kuhusu bei ya mbolea Naibu Waziri, Mavunde ameishukuru mamlaka kwa miongozo na ushauri inayotoa kwa serikali ikiwa ni pamoja na kushauri kuhusu umuhimu



Naibu Waziri wa Kilimo Anthony Mavunde akisaini kitabu cha wageni mara baada ya kufika katika ofisi ya Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo (hayupo pichani) mwishoni mwa mwezi Februari ili kukagua maendeleo ya ujenzi wa maabara ya mbolea unaosimamiwa na mamlaka hiyo.

# TFRA yapongezwa usimamizi ujenzi maabara ya mbolea

wa kuwa na maabara hii na kusimamia ujenzi wa kiwanda cha mbolea cha intracom kinachojengwa Jijini Dodoma.

Alisema ujenzi wa kiwanda cha mbolea cha Intracom umefikia asilimia 65 huku kikitarajiwa kuanza uzalishaji wa tani 6000 za mbolea kwa mwaka na uzalishaji wake kuanza mwezi wa Julai na hivyo kupunguza mzigo wa gharama ya mbolea kwa wakulima katika msimu ujao wa kilimo.

Akizungumzia kuhusu maabara hiyo Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA Dkt. Stephan Ngailo ali sema maabara hiyo itakuwa na viwango vya kimataifa na ni maabara pekee Afrika Mashariki na Kati katika upimaji wa sampuli za mbolea.

Alisema mara ujenzi wake utakapokamilika mamlaka itahakikisha maabara hiyo imepata ithibati ya kimataifa ili uchambuzi wake utambulike duniani kote na kubainisha kuwa tayari taratibu za kufikia hazma hiyo zimeshaanza.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mradi huo Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa maabara hiyo, Bi. Mwahija Irika alisema ujenzi huo umefikia asilimia 51 ambapo ujenzi wa kuta na umwagaji zege la juu katika ghorofa ya kwanza umekamilika.

Amesema, nguzo katika ghorofa ya pili zimekamilika na kwamba kazi inayoendelea kwa sasa ni ufungaji wa marine board na mbao kwa ajili ya kumwaga zege katika ghorofa ya kwanza.

Akihitimisha taarifa yake Bi. Mwahija aliishukuru Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa juhudi kubwa za kuisaidia mamlaka kupata eneo la ujenzi pamoja na ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha ujenzi huo unakamilika kwa wakati.






Matukio mbalimbali wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde akikagua maendeleo ya ujenzi wa maabara ya mbolea.

# Wazalishaji wadogo mbolea wajengewa uwezo, waoneshwa fursa kujipatia mikopo



Kaimu Meneja wa Uzalishaji wa Ndani na Mazingira wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Stephenson Ngoda akiongea jambo wakati wa semina kwa wazalishaji wadogo wa mbolea nchini iliyoandaliwa na mamlaka hiyo kwa lengo la kuwaongezea uwezo ili wazalishe kwa viwango vinavyokubalika na kuwaongezea tija.

Imeelezwa kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) ipo katika kampeni ya kuwawezesha wazalishaji wadogo wa mbolea nchini kuongeza kiwango cha uzalishaji ili kukidhi mahitaji ya mbolea nchini ambapo kwa sasa ni asilimia kumi ya mahitaji ya mbolea inazalishwa nchini na kiasi kinachobaki kinatoka nje ya nchi.

Hayo yamebainishwa tarehe 15 Februari, 2022 na Kaimu Meneja wa Uzalishaji wa Ndani na Mazingira, Stephenson Ngoda alipokuwa akifungua mafunzo kwa wazalishaji wadogo wambolea nchini yaliyolenga kuwajengea uwezo wa kimtaji na kitekinolojia ili kuendeleza shughuli za uzalishaji kwa tija.

Ngoda amebainisha kuwa agenda kubwa kitaifa ni kuongeza uzalishaji wa ndani wa mbolea ili kukidhi mahitaji ya wakulima na kukiri kuwa rasilimali kwa ajili ya uzalishaji wa mbolea nchini upo.

Amesema mafunzo hayo yanaumuhimu mkubwa katika kuwawezesha wazalishaji wa ndani kuzalisha mbolea bora kwa tija ili kupunguza utegemezi wa viwanda vya nje ambapo kufuatia mlipuko wa Ugongwa wa Covid 19 bei ya mbegu imepanda na kusababisha changamoto kubwa kwa wakulima kuweza kumudu bei ya mbolea sokoni.

Akizungumza katika kikao hicho Esther Kapakala amesema TFRA imeamua kufanya mafunzo hayo kanda ya Kaskazini kutokana na kuwa na wazalishaji wengi wa mbolea waliojikita

# Wazalishaji wadogo mbolea wajengewa uwezo, waoneshwa fursa kujipatia mikopo

katika uzalishaji wa mbolea za maji (Folier Fertilizer) pamoja na mbolea ngumu ili kuwawezesha kutatua changamoto za kimtaji na kiteknolojia.

Amesema, wazalishaji wengi wamekuwa na changamoto za miundombinu duni na mitaji hivyo kikao hicho kinawakutanisha wazalishaji hao na watoa huduma za kifedha ili kuwawezesha kupata mitaji na teknolojia bora itakayowawezesha kuzalisha kwa tija.



Kaimu Meneja wa Uzalishaji wa Ndani na Mazingira wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Stephenson Ngoda na Kaimu Meneja wa Kanda ya Kaskazini Gothard Liampawe, wakiteta jambo wakati wa mafunzo kwa wazalishaji wadogo wa mbolea yaliyokuwa yakifanyika katika ukumbi wa Chuo cha Afya Arusha (CEDHA).

Kwa upande wake mwezeshaji kutoka SIDO Nina Nchimbi amewataka wazalishaji wa mbolea kutafuta taarifa sahihi zinazohusiana na shughuli zao ili kuongeza tija katika uwekezaji wao na zaidi kupata ufumbuzi wa changamoto za mitaji zinazowakabili.

Amesema shilika lake lipo kwa lengo la kuwasaidia kuwapa ushauri katika uanzishaji wa viwanda vyao lakini pia inawarahisishia katika usajili wa bidhaa wanazozalisha na hivyo bidhaa zao kudhibitishwa na TBS kwa wakati tofauti na wajasiriamali ambao hawajapitia kwao ili kupata ushauri wa namna ya kuandaa bidhaa zao.



Meneja wa Shirika la Viwanda Vidogovidogo Nchini (SODO) Nina Nchimbi akitoa mada wakati wa mafunzo kwa wazalishaji wadogo wa mbolea yaliyofanyika tarehe 15 Februari, 2022 katika ukumbi wa Chuo cha Afya Arusha (CEDHA).

Pamoja na mwezeshaji kutoka sido walikuwepo wengine kutoka NMB, CRDB, PASS, EFTA ambapo wote walieleza msaada wa kitaalamu wanayoitoa kwa wakulima ikiwa ni pamoja na uandishi wa maandiko ya biashara inayowawezesha kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha, kuwakopesha vifaa au mitambo, na kuwapa ushauri wa kitaalamu katika uzalishaji wa mbolea ili kukidhi viango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

# TFRA yamtaka mkandarasi kuongeza kasi ujenzi maabara ya mbolea



Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa Maabara ya Mbolea Joseph Charos (kushoto) akiambatana na Msimamizi wa Ujenzi Hamza Said (katikati) walipokuwa wakikagua maendeleo ya ujenzi wa mradi huo.

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imemtaka mkandarasi anayejenga maabara ya mbolea kuongeza kasi ya ujenzi ili kukamilisha mradi huo kwa wakati.

Hayo yameelezwa leo tarehe 03 Februari, 2022 na mwenyekiti wa Kamati ya ujenzi wa maabara hiyo Bw. Joseph Charos alipotembelea eneo la ujenzi kwa lengo la kujionea hatua ya maendeleo ya ujenzi huo.

Charos ambaye pia ni Kaimu Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja amemtaka mkandarasi kuzingatia ujenzi wenye ubora unaotakiwa ili kukidhi viwango vya kimataifa.

Ujenzi wa maabara hiyo unaotekelezwa na Chuo cha Ufundi Arusha (ATC) unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2022 ambapo itakuwa na ubora wa kimataifa ili kuweza kuhudumia wateja wa ndani na nje ya nchi.

Charos amemuagiza msimamizi huyo kuanza shughuli za ujenzi mapema kabla jua halijatoka ili mafundi wafanye kazi wakiwa na nguvu na kubainisha kuwa jua linachochea uchovu wa mwili na hivyo kuwafanya mafundi kutokuwa na nguvu ya kufanya kazi kwa nguvu.

Kwa upande wake, Bw. Hamza amekiri kupokea na kufanyia kazi maelekezo hayo na kuahidi kuwa ujenzi wa mradi huo utakamilika mapema mwezi Mei, 2022 na kubainisha kuwa hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 50.

Kukamilika kwa maabara hiyo inayosimamiwa na TFRA kutasaidia kuharakisha shughuli za upimaji wa sampuli za mbolea na kuboresha huduma ya upimaji wa mbolea zote zinazotengenezwa ndani na nje ya nchi.



Msimamizi wa Ujenzi Hamza Said (kushoto) akieleza ujenzi wa maabara ya mbolea unavyoendelea kwa wajumbe wa Kamati ya Ujenzi huo. Wa pili kulia ni Mwenyekiti wa kamati hiyo Joseph Charos.



Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa Maabara ya Mbolea Joseph Charos (kushoto) akitoa maelekezo kwa msimamizi wa maabara ya mbolea Hamza Said kamati ilipotembelea kukagua maendeleo ya ujenzi wa maabara hiyo.

# Shirika la Posta lawanoa watumishi TFRA

Leo tarehe 2 Februari, 2022 Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Victoria Elangwa amepokea ujumbe wa wataalamu kutoka Shirika la Posta Tanzania waliofika kutoa elimu ya huduma zao kwa watumishi wa TFRA.

Baada ya mapokezi, wataalamu hao wakiongozwa na Meneja wa Utawala (TFRA) Naomi Fwemula walikutana na kuzungumza na watumishi juu ya huduma zinazotolewa na shirika la Posta na kuwasihi watumishi kutumia huduma zinazotolewa na Shirika hilo.

Akizungumza katika kikao hicho, Adrew Liundi, Afisa Masoko kutoka posta amesema huduma zinazotolewa na shirika hilo ni pamoja na Usafirishaji wa nyaraka, vifurushi, huduma za uhamisho, online shopping pamoja na posta kiganjani.




Mkurugenzi wa Huduma za Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Victoria Elagwa akiwa katika picha na wataalamu kutoka shirika la posta waliofika katika ofisi za mamlaka ili kueleza huduma zinazotolewa na shirika hilo. Wa kwanza kushoto ni Kaimu Meneja wa Utawala Naomi Fwemula



Watumishi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) wakifuatilia mada inayotolewa na wataalamu wa shirika la posta Tanzania



Meneja wa Biashara wa Shirika la Posta Tanzania akieleza jambo kwa watumishi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) walipofika katika ofisi za mamlaka hiyo ili kueleza majukumu yao na huduma zinazotolewa kwa wateja.

# Watumishi wapya TFRA watakiwa kuzingatia maadili ya Utumishi wa Umma

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo amewataka watumishi waliohamia katika mamlaka hiyo kutoka, halmashauri, wizara na taasisi nyingine za serikali kutekeleza majukumu yao kwa weledi huku wakizingatia maadili ya utumishi wa umma.

Dkt. Ngailo ametoa wito huo tarehe 09 Februari, 2022 alipokuwa akifungua mafunzo kwa watumishi hao yaliyolenga katika kuwapa uelewa wa majukumu yanayotekelezwa na TFRA hivyo kuwarahisishia watakapokuwa katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Akiyataja maadili hayo, Dkt. Ngailo amesema ni pamoja na uaminifu, utunzaji wa siri za ofisi, kutojihusisha na ulevi wakati wa kazi, kujituma katika kazi, kuepuka kujihusisha na masuala ya rushwa.

Akisisitiza jambo kuhusu rushwa, Dkt. Ngailo amesema rushwa ni adui wa haki na inaathiri sana utendaji wa kazi kwa mtoaji na mpokeaji wa rushwa na kuwahakikishia watumishi hao kuwa kitakachozingatiwa katika ofisi hiyo ni utendaji mzuri wa kazi na si vinginevyo.

Akizungumzia suala la ulevi, Dkt. Ngailo amewataka watumishi hao kujiepusha na masuala ya unywaji wa pombe na ulevi wakati wa kazi na kwamba kujihusisha na jambo hilo kutawafanya kutokidhi vigezo vya kutumika katika mamlaka hiyo.

Aidha, Dkt. Ngailo amewataka watumishi waliopangwa kutekeleza majukumu yao katika ofisi za kanda kuhakikisha wanaimarisha mahusiano baina ya ofisi yao (TFRA - kanda) na halmashauri pamoja na wadau wengine wa mbolea popote nchini.

Pamoja na hayo amewataka watumishi hao kuwa mawakili wazuri katika kutumia rasilimali za umma ikiwa ni pamoja na magari na samani zinazotumika katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Ushirikiano na mipango mizuri katika utekelezaji wa majukumu utasaidia katika kuhakikisha rasilimali za serikali zinatumika vizuri. Dkt. Ngailo alisisitiza.

Akizungumzia majukumu



Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) akizungumza na watumishi wapya wa Mamlaka hiyo alipokuwa akifungua mafunzo yaliyojenga kuwapa uelewa wa majukumu ya mamlaka ili kurahisisha katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.



Kaimu Meneja wa Uzalishaji wa Ndani na Mazingira, Stephenson Ngoda akiwapitisha watumishi katika majukumu ya kitengo anachokisimamia ili kuwapa uelewa watumishi waliohamia kutumika katika ofisi hiyo.

# Watumishi wapya TFRA watakiwa kuzingatia maadili ya Utumishi wa Umma



Kaimu Meneja wa Huduma za Sheria Janeth Mugini akiwasilisha mada juu ya majukumu ya kitengo chake katika kutoa huduma za kisheria katika Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea kwa watumishi waliohamia utumishi katika mamlaka hiyo.

ya TFRA Dkt. Ngailo alisema ni udhibiti wa mbolea, uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima, kutoa ushauri kwa serikali kuhusu masuala yanayohusiana na mbolea, kushirikiana na wadau wengine katika masuala yote yanayohusiana na mbolea na kushirikiana na mamlaka nyingine za serikali katika kuhakikisha mbolea inawafikia wakulima kwa wakati.

Akizungumza wakatiwa uwasilishaji wa mada DRS Gerod Nganilevanu alisema awali udhibiti wa mbolea ulikuwa ukisimamiwa na tbs na kuonekana kutokidhi mahitaji ya wakulima kwa wakati na hivyo Serikali kuona umuhimu wa kuanzisha mamlaka itakayosimamia na kuhakikisha inarahisisha upatikanaji wa mbolea inayokidhi viwango na kwa wakati.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Pamoja Stevenson Ngoda alisema idara yake ina jukumu kubwa la kuhakikisha inaratibu masuala ya ununuzi wa pamoja wa mbolea pamoja na kuhamasisha uzalishaji wa ndani wa mbolea ili kuwapunguzia wakulima mzigo wa kununua mbolea zilizoingizwa kutoka nje ya nchi kwa gharama kubwa.

Wakati huohuo akiwasilisha mada kwa niaba ya Meneja wa Huduma za Sheria Janet Mugini alisema kitengo chao kinajihusisha kutoa huduma na ushauri wa kisheria na kuhakikisha mamlaka inaendeshwa kwa mujibu wa sheria kama ilivyokusudiwa

Kwa upande wake, Afisa Tehama aliwapitisha watumishi hao kwenye mfumo unaotumiwa na mamlaka hiyo katika masuala ya usajili wa wafanyabiashara, wazalishaji na wasambazaji wa mbolea nchini.

Amesema jukumu kubwa la kitengo cha tehama ni kusimamia mifumo yote ya tehama inayotumika katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya mamlaka hiyo

Mwisho Kaimu Meneja wa idara ya Mipango na Upelemaji George Lugome amesema lengo kuu la TFRA ni kuhakikisha mbolea inayokidhi viwango i awafikia wakulima kwa wakati na kwa bei wanayoweza kuimudu.

Amesema kutokana na mbolea kupanda kwenye soko la dunia kwa mwaka huu imeathiri soko la mbolea kwenye soko la dunia ambapo mamlka inafanyia kazi kuona namna bora ya kuwawezesha wakulima kupata mbolea kwa msimu wa kilimo.

Naye Meneja wa Kitengo cha Manunuzi, Joseph Hilary amewataka watumishi hao kuzingatia taratibu za manunuzi wakati wote wa utumishi wao ili kuepuka migogoro isiyokuwa ya lazima

Mafunzo hayo ni kwa mujibu wa miongozo ya utendaji wa Mamlaka yanayofanyika kwa siku tatu kuanzia leo tarehe 9 hadi tarehe 11 Februari, 2022.

# Watumishi TFRA watakiwa kufuata miongozo ya Mamlaka katika utendaji



Mkurugenzi wa Huduma za Mamlaka, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Victoria Elangwa akizungumza na wakati akifunga mafunzo yaliyofanyika kwa siku 3 katika ukumbi wa mkutano watumishi wapya wa Mamlaka wa malaka hiyo.

Ikiwa ni siku ya pili ya mafunzo kwa watumishi waliohamishiwa kutumika katika Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi Victoria Elangwa amewataka watumishi hao kufuata miongozo ya taasisi katika kutekeleza majukumu yao ili maamuzi yawe na mlengo wa kuinua taasisi na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Akiwasilisha mada katika darasa hilo Afisa Rasilimali Watu, Ruth Magesa amekabidhi miongozo yote inayotumika katika utendaji kazi wa mamlaka hiyo kwa watumishi hao ili waweze kuitumia kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Miongoni mwa miongozo iliyotolewa na Mamlaka ni pamoja na Sera ya Ukimwi na Magonjwa yasiyo ya kuambukiza (HIV and NCD), Muundo na Majukumu ya Mamlaka yaliyoidhinishwa, Sera ya kufichua maovu, Sera ya malalamiko, muongozo wa zawadi na ukarimu na mingineyo.

Pamoja na kugawa miongozo hiyo, Magesa amewataka watumishi hao kuzingatia mtiririko wa majukumu na uongozi katika utendaji wao wa kila siku.

Kwa upande wake, Kaimu



Kaimu Meneja wa Sehemu ya Utawala na Rasilimali Watu Naomi Fwemula akimkaribisha Mkurugenzi wa Huduma za Mamlaka, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Victoria Elangwa ili kufunga mafunzo yaliyokuwa yakitolewa kwa watumishi wapya wa mamlaka hiyo hivi karibuni.

# Watumishi TFRA watakiwa kufuata miongozo ya Mamlaka katika utendaji



Afisa Utumishi Ruth Magesa (kulia) akitoa elimu juu ya maadili ya mtumishi wa Umma kwa watumishi wapya wa Mamlka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA).

Meneja wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani Pauline Mganga amewataka watumishi hao kuimarisha ushirikiano baina yao na kitengo hicho ili kuweza kutatua na kueleweshana namna bora ya kutekeleza majukumu kwa mujibu wa sheria na taratibu zinazoisimamia mamlaka.

Amesema, kazi ya kitengo hicho katika mamlaka hiyo na nyingine ni kukagua namna idara na vitengo vinavyotekeleza majukumu yake na kuishauri mamlaka ili iweze kusimamia sheria na taratibu kikamilifu.

Akihitimisha mafunzo hayo kwa siku ya pili Kaimu Meneja wa Kitengo cha Rasilimali watu Naomi Fwemula aliwashukuru watoa mada na viongozi wakuu wa taasisi kwa elimu iliyotolewa kwa watumishi hao.

Aidha, amewashukuru na kuwatakia utekelezaji mwema wa majukumu katika vituo vyao vipya vya kazi.

Wakati huohuo Joshua Ngondya Kaimu Meneja Kanda ya Kati, akizungumza kwa niaba ya watumishi wengine ameishukuru mamlaka kwa kuandaa utaratibu wa mafunzo na kukiri kuwa wamepata mwanga wa namna ya kwenda kutekeleza majukumu yao katika vituo vyao vya kazi.

Mafunzo hayo ni ya siku tatu yaliyoanza jana tarehe 9 hadi tarehe 11 Februari ambapo leo yamehitimishwa rasmi kwa waajiliwa wageni na siku ya mwisho mafunzo yatahusisha watumishi wote wa TFRA ili kuwapa uelewa katika suala la Maadili katika Utumishi wa Umma.



Matukio mbalimbali wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde akikagua maendeleo ya ujenzi wa maabara ya mbolea.





Matukio mbalimbali wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde akikagua maendeleo ya ujenzi wa maabara ya mbolea